# Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Wakulima (WFO) Wakamilika na Wito kwa Uzingatiaji wa Kilimo Endelevu Kinacholenga Mkulima

**Na Friday Phiri**

**LIVINGSTONE, Zambia, Mei 9 2016 (IPS) -** Zaidi ya wajumbe 600, wanaowakilisha angalau wakulima 570 waliotawanyika kote ulimwenguni, walikutana nchini Zambia kutoka Mei 4-7, ili kujadili ustawi wa wakulima.

Miongoni mwa wajumbe wa Zambia ni Mary Nyirenda, mkulima anayeibuka kutoka Livingstone. "Nina shamba lenye eka 35 lakini ninatumia eka 5 pekee kutokana na uhaba wa maji. Nina kisima kimoja, na ninaweza kunyunyuzia maji sehemu ndogo pekee ya shamba langu. Nilikufaa mwoyo kungojea mvua ya msimu wa 2013/14 wakati nilipoteza eka tano za mahindi kutokana na kiangazi, "Nyirenda alielezea IPS.

Nyirenda alibahatika kuwa sehemu ya Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Wakulima, matarajio ya Nyirenda yalikuwa ni kujifunza mbinu bunifu za jinsi ya kuboresha uzalishaji wa mazao yake na kupata soko la mazao yake na kuku anaowafuga. Lakini je, mkutano huu ulitimiza matarajio yake?

"Ndiyo mkutano huu umetimiza matarajio yangu, hasa katika sehemu ya kupata masoko ya kuuza mazao yangu. Nimejifunza kwamba kufanya kazi kama kikundi kunatupa sauti thabiti na uwezo wa kujadiliana kuhusu bei za mazao yetu. Nimekuwa nikijitahidi mimi pekee yangu lakini kwa sasa ninaelewa kwamba watu wawili wakiungana pamoja ni afadhali kuliko mmoja anayepigania jambo fulani, kwa hivyo, jukumu langu nikitoka hapa ni kuimarisha ushirikiano wetu ambao sio thabiti baina ya wazalishaji mazao," Nyirenda alisema, huku akisisitiza uwezo unaoletwa na mashirika ya wakulima- ambayo Shirika la Kimataifa la Wakulima ni kielelezo.

Mkutano huu uliongozwa na mada kuu ya 'Ushirikiano wa Kukuza Uchumi'. Mwaka huu Mkutano wa Kimataifa wa Shirika la Kimataifa la Wakulima (WFO) ulijadili nguzo nne za kukuza maendeleo ya kilimo ambazo ni:

mabadiliko ya hali ya anga, umiliki wa ardhi, ubunifu na kukuza uwezo wa wazalishaji chakula.



*Mary Nyirenda akiwa katika shamba lake mjini Livingstone, Zambia. Picha ni kwa Hisani ya: Friday Phiri/IPS*

Mwito wa wajumbe wote katika mkutano huo ni kubadili maelezo kwamba wakulima ndio miongoni mwa watu maskini sana duniani ilhali wakulima ndio kijenzi muhimu cha sekta ya chakula ya mabilioni ya dola wenye jukumu la kuilisha dunia yote.

Rais wa Shirika la Kimataifa la Wakulima, Evelyn Nguleka anasema kuwa hali hii inahitaji kubadilika. "Ni kweli kwamba karibu maeneo yote ya dunia wakulima ndio wanaunda kundi la watu maskini, lakini swali ni, kwa nini hali hii?" Nguleka alishangaa alipokuwa anaongea katika mkutano na Waandishi wa Habari wakati wa kufungwa kwa Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Wakulima.

Alisema kuwa mkutano ulifafanua kuwa ukosefu wa mpangilio na ukosefu wa maelezo ndio sababu ya hali hii ya wakulima ya 'kukosa maendeleo', ikizingatiwa kwamba "ikiwa wakulima watasalia katika hali ya kutengwa wataendelea kuwa maskini."

"Hii ndio sababu tunaandaa chombo cha kisheria cha ukulima wa mkataba, ambacho mara nyingi kimewafaa wakulima wadogo wadogo ambao maarifa yao kuhusu masuala ya kisheria ni ya kiwango cha chini mno na mara nyingi huadaiwa," David Velde ambaye ni Rais wa Shirika la Kitaifa la Wakulima Nchini Marekani (National Farmers Union) na mwanachama wa bodi ya Shirika la Kimataifa la Wakulima alisema.

Velde aliiambia IPS kuwa zana mbalimbali zingehitajika ili kuwasaidia wakulima wadogo ili waweze kunufaika kikamilifu kutokana na kazi zao, hasa katika ulimwengu unaopitia mabadiliko ya hali ya anga, mada ndogo ambayo haikukosa kujadiliwa katika mkutano huu, kutokana na athari zake kubwa.

Na uhamishaji wa teknolojia unaozingatiwa kama kipengele muhimu katika ajenda ya maendeleo endelevu kama ilivyobainishwa katika mkataba wa Paris wa mabadiliko ya hali ya anga, wajumbe walitambua kwamba uvumbuzi na ujenzi wa rasilimali watu ya wakulima ili kuboresha uzalishaji chakula, hauwezi kujadiliwa katika ombwe tupu.

"Kilimo kwa kweli ni sekta muhimu ambayo inahitaji kuzingatiwa kwa makini zaidi. Ukweli ni kwamba mashirika ya wakulima duniani yapo na hii ni ishara kwamba masuala ya uzalishaji wa chakula, usalama wa chakula, mabadiliko ya hali ya anga ni masuala ya kimataifa ambayo hayawezi kushughulikiwa bila kuhusisha watu wengi. Wakulima wanahitaji maelezo kuhusu mbinu na teknolojia bora za jinsi ya kukuza uzalishaji mazao katika njia inayozingatia ufahamu wa mabadiliko ya hali ya anga, " Rais wa Zambia, Edgar Lungu, alisema katika hotuba yake kwa Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Wakulima.

Katika harakati za dunia za kuwalisha watu milioni 793 kufikia mwaka wa 2030, na makadirio ya ongezeko la watu kufikia hadi wa bilioni 9.6 ifikapo mwaka wa 2050, zaidi ya nusu ya idadi hii ya watu ikiwa barani Afrika, Shirika la Kimataifa la Wakulima lina jukumu la kuchangia katika kuboresha hali hii kutoka na wajibu ambao wanachama wake wanaubeba, ambao unaweza kutimizwa tu kupitia ongezeko la uzalishaji chakula.

"Shirika la Kimataifa la Wakulima linatambua kwamba kuna masuala mawili yanayokinzana ambayo ni -kuwalisha watu duniani na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga. Majukumu haya mawili yanahitaji rasilimaili nyingi lakini tunaamini kwamba inawezekana kukabiliana na changamoto hizi mbili kupitia ongezeko katika uzalishaji chakula kwa kutumia teknolojia ya kisasa, "William Rolleston, Rais wa Shirikika la Wakulima la New Zealand, alisema.

Rolleston, ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Shirika la Kimataifa la Wakulima aliambia IPS kwamba kazi ya Shirika la Kimataifa la Wakulima

haijumuishi kuwafadhili wakulima, bali ni kuwasaidia wanachama wake kuvumbua na kubuni ushirikiano kwa madhumuni ya ukuaji wa kilimo.

Imetambulika kwa muda mrefu kwamba kimataifa, mabadiliko ya hali ya anga ikiwa hayatakabiliwa, yanaweza kuwa kikwazo katika hatua za kuafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals -SDGs). Hali hii kwa sasa, inawasilisha uamuzi mkubwa ambao viongozi wa mataifa ya dunia wanahitaji kufanya- kukumbana na mabadiliko ya hali ya anga, na athari kubwa kwa uwezo wa dunia wa kuzalisha chakula, ambao miaka nenda miaka rudi umetegemea zaidi matumizi ya kaboni kutokana na athari zake za kiuchumi.

Kwa kuidhinisha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika mkataba wa kihistoria wa mwaka uliopita, ajenda ya kijamii na kiuchumi ya dunia inatarajiwa kubadilishwa kabisa. Hata hivyo, rais wa Shirika la Kimataifa la Wakulima, Evelyn Nguleka anataka wakulima wasalie kuwa lengo la uundaji wa sera duniani:

"Chochote kitakachobadilishwa ili dunia isonge mbele, kisifanywe kwa kuwatilia wakulima gharama zaidi za kuishi na kupata faida kutokana na mazao yao, Evelyn alisisitiza.

Kwa Nyirenda, upatikanaji wa masoko ya kuuza mazao yake ndio muhimu kwa uwezo wa wakulima kuzalisha mazao, hasa kwa wanawake, ambao kulingana na Shirika la Umoja wa Kimataifa la Chakula na Kilimo (FAO) wanajumuisha 50% ya wafanyakazi wote katika kilimo, lakini barani Afrika idadi hii ni kubwa zaidi- idadi hii ni 80%.

"Utangamano wangu na mashirika ya kimataifa kama vile Halmashauri ya Kimataifa ya Ufadhili wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na mashirika mengine ambayo yana nia ya kuwawezesha wanawake, ulikuwa ni ufunguo mkubwa wa namna ya kusonge mbele," Nyirenda alisema.

(Mwisho)